Udanganyifu Wa Waalimu Wa Uongo

na

Ellis P. Forsman

Udanganyifu Wa Waalimu Wa Uongo

na

Ellis P. Forsman

Oktoba 15, 2011

Udanganyifu Wa Waalimu Wa Uongo

2 Pet. 2:18-22

Onyo la Petro kuhusu "*waalimu wa uongo*" mwanzo wa kifungu hiki cha waraka wa pili inajumuisha maelezo ya:

Uharibifu wa waalimu wa uongo.

2 Pet. 2:1-3, "*Lakini kuliondokea manabii wa uongo katika wale watu, kama vile kwenu kutakavyokuwako waalimu wa uongo, watakaoingiza kwa werevu uzushi wa kupoteza, wakimkana hata Bwana aliyewanunua, wakijiletea uharibifu usiokawia. Na wengi watafuata ufisadi wao; na kwa hao njia ya kweli itatukanwa. Na katika kutamani watajipatia faida kwenu kwa maneno yaliyotungwa; ambao hukumu yao kwanzia zamani haikawii, wala uvunjifu wao hausinzii.*"

Maangamizi ya waalimu wa uongo.

2 Pet. 2:4-9, "*Kwa maana ikiwa Mungu hakuwaachilia malaika waliokosa, bali aliwatupa shimoni, akawatia katika vifungo vya giza, walindwe hata ije hukumu; wala hakuuachilia ulimwengu wa kale, bali alimuhifadhi Nuhu, mjumbe wa haki, na watu wengine saba hapo alipoleta Gharika juu ya ulimwengu wa wasiomcha Mungu; tena akaihukumu miji ya Sodoma na Gomora, akiipindua na kuifanya majivu, akaifanya iwe isha kwa watu watakaokuwa hawamchi Mungu baada ya haya; akamwokoa Lutu, yule mwenye haki aliyehuzunishwa sana na mwenendo wa ufisadi wa hao wahalifu; maana mtu huyu mwenye haki akikaa kati yao, kwa kuona na kusikia, alijitesa roho yake yenye haki, siku baada ya siku, kwa matendo yao yasiyo na sheria; basi, Bwana ajua kuwaokoa watauwa na majaribu, na kuwaweka wasiyo haki katika hali ya adhabu hata siku ya hukumu.*"

Machafuko ya waalimu wa uongo.

2 Pet. 2:10-17, "*Na hasa wale waufuatao mwili katika tamaa ya mambo machafu. Na kudharau mamlaka. Wenye ushupavu, wenye kujikinai, hawatetemeki, wakiyatukana matukufu; ijapokuwa malaika ambao ni wakuu zaidi kwa uwezo na nguvu, hawaleti mashtaka juu yao mbele za Bwana. Lakini hao kama wanyama wasio na akili, ambao walizaliwa kama wanyama tu wa kukamatwa na kupotezwa, wakikufuru katika mambo wasiyoyajua, wataangamizwa katika maangamizo yao; wakipatikana na madhara, ambao ni ujira wa udhalimu wao, wakidhania kuwa ulevi wakati wa mchana ni anasa; wamekuwa ni mawaa na aibu*

wakifuata anasa zisizo kiasi katika karamu zao za upendo, wafanyapo karamu pamoja nanyi; wenye macho yajaayo uzinzi, watu wasio koma kutenda dhambi, wenye kuhadaa roho zisizo imara, wenye mioyo iliyozoezwa kutamani, wana wa laana; wakiiacha njia iliyonyoka, wakapotea, wakiifuata njia ya Balaamu, mwana wa Beori, aliyependa ujira wa udhalimu; lakini alikaripiwa kwa uhalifu wake mwenyewe; punda, asiyeweza kusema, akinena kwa sauti ya kibinadamu, aliuzuia wazimu wa nabii yule. Hawa ni visima visivyo na maji, na mawingu yachukuliwayo na tufani, ambao weusi wa giza ni akiba waliyowekewa."

Mustari wa 17 unafupisha uharibifu wao kwa kuwaelezea kama…

- "*Visima visivyo na maji.*"
- "*Mawingu yachukuliwayo na tufani.*"

Ikimaanisha kwamba wanapo ahidi mengi, kwa hakika hawatowi kile walichokiahidi.

Hivyo ni "wachafuzi"; na machafuko ya waalimu wa uongo huonekana zaidi tunapozingatia sehemu ya mwisho ya sura ya pili.

2 Pet. 2:18-22, "*Maana wakinena maneno makuu mno ya kiburi, kwa tamaa za mwili na kwa ufisadi uwahadaa watu walioanza kuwakimbia wale wanaoenenda kwa udanganyifu; wakiwaahidia uhuru, nao wenyewe ni watumwa wa uharibifu, maana mtu akishindwa na mtu huwa mtumwa wa mtu yule. Kwa maana wale waliokwisha kuyakimbia macha ya dunia kwa kumjua Bwana na Mwokozi Yesu Kristo, kama wakinaswa tena na kushindwa, hali yao ya mwisho imekuwa mbaya kuliko ile ya kwanza. Maana ingekuwa heri kwao kama wasingaliijua njia ya haki, kuliko kuijua kasha kuiacha ile amri takatifu waliopewa. Lakini imetukia kwao sawasawa na ile mithali ya kweli, Mbwa ameyarudia matapiko yake mwenyewe, na nguruwe aliyeoshwa amerudi kugaagaa matopeni.*"

Mistari ya 18-22 inaonyesha wazi jinsi hawa "*waalimu wa uongo*" walivyo wadanganyifu, wakianza na…

Ni waongo katika mifumo yao

Wanatumia maneno ya uongo.

Petro ameonya mapema:

2 Petr. 2:3, "*Na katika kutamani watajipatia faida kwenu kwa maneno yaliyotungwa; ambao hukumu yao tangu zamani haikawii, wala uvunjifu wao hausinzii.*"

"Watawalipua kwa maneno ya uongo".

Sasa anasema:

2 Pet. 2:18, "*Maana wakinena maneno makuu mno ya kiburi, kwa tamaa za mwili na ufisadi huwahadaa watu walioanza kuwakimbia wale wanaoenenda katika udanganyifu;*"

"Wakinena maneno makuu mno ya bure."

Wakitumia maneno matamu na yenye ahadi, bali inakosa kitu halisi.

Kwa hakika wanauvutia mwili.

Hivyo waongo ni hawa waalimu, mtu anaweza kufikiria kwamba wanawapata watu kutokana na mafundisho yao.

Bali malengo yao ni katika "*tama ya mwili*".

Ambayo inaweza kujumlisha vitu kama ufisadi, mambo ya kimwili, wivu, kiburi.

- Gal. 5:19-21, "*Basi matendo ya mwili ni dhahiri ndiyo haya, uasherati, uchafu, -ufisadi, ibada ya sanamu, uchawi, uadui, ugomvi, wivu, hasira, fitina, faraka, uzushi, husuda, ulevi, ulafi, na mambo yanayofanana na hayo, katika hayo nawaambia mapema, kama nilivyo kwisha kuwaambia, ya kwamba watu watendao mambo ya jinsi hiyo hawataurithi ufalme wa Mungu.*"
- 1 Yoh. 2:15-17, "*Msiipende dunia wala mambo yaliyomo katika dunia. Mtu akipenda dunia, kumpenda Baba hakumo ndani yake. Maana kila kilichomo duniani, yaani, tamaa ya mwili, na tamaa ya macho, na kiburi cha uzima, havitokani na Baba, bali vyatokana na dunia. Na dunia inapita, pamoja na tamaa zake, bali yeye afanyaye mapenzi ya Mungu adumu hata milele.*"

Hivyo, wanatoa ahadi ambazo hakika inaonyesha kile ambacho ni mapenzi ya mwili.

Siyo swala kwa wale wanaoahadi "afya na mali" pamoja na injili?

Pia ni "*kupitia tamaa iliyozidi*" kwamba hawa waalimu wanarubuni nafsi ambazo hazipo imara.

Tamaa iliyozidi kwa Kiyunani ni aselgeia {as-elg'-i-a} ikimaanisha tamaa "isiyozuilika, iliyokithiri, uchafu, aibu"

Kwa aibu wanaingiza tamaa zao za mwili, wanapoipitisha kama kitu cha maana.

Wanaonyesha utajiri uliokithiri kama kitu ambacho mtu anaweza kutegemea kuupokea kama mfuasi wa mafundisho yao.

Kupitia mifumo hii ya uongo, wanatafuta kuwanasa wale ambao "wamekimbia kutoka kwa wale wanaoishi katika makosa".

2 Pet. 2:18, "*Maana wakinena maneno makuu mno ya kiburi, kwa tamaa za mwili na kwa ufisadi huwahadaa watu walioanza kuwakimbia wale wanaoenenda katika udanganyifu.*"

Hii inatupeleka katika kipengele kingine cha Petro…

Ni waongo katika ahadi zao

Wanaahidi "*uhuru*", lakini hawatowi.

2 Pet. 2:19, "*Wakiwaahidi uhuru, nao wenyewe ni watumwa wa uharibifu, maana mtu akishindwa na mtu huwa mtumwa wa mtu yule.*"

Hasa, kama ni uhuru utokao katika "tamaa za mwili".

Kama jinsi tulivyoona, wanafanya mitego yao kupitia "tamaa za mwili".

- 2 Pet. 2:1, "*Lakini kuliondokea manabii wa uongo katika wale watu, kama vile kwenu kutakavyokuwako waalimu wa uongo, watakaoingiza kwa werevu uzushi wa kupoteza, wakimkana hata Bwana aliyewanunua, wakijiletea uharibifu usiokawia.*"
- 2 Pet. 2:18, "*Maana wakinena maneno makuu mno ya kiburi, kwa tama za mwili na kwa ufisadi huwahadaa watu walioanza kuwakimbia wale wanaoenenda katika udanganyifu;*"

Hivyo, huwatia mateka kupitia kile walichowaahidi.

Wanaahidi "*uhuru*" wakati wao wenyewe ni mateka.

Kuna "watumwa wa uharibifu" wakijaribu kuahidi kile wasicho nacho.

Kama uthibitisho wa "uharibifu wao", tayari tumeshaona…

Wanajaribu kuangamiza kupitia tama.

2 Pet. 2:3, "*Na katika kutamani watajipatia faida kwenu kwa maneno yaliyotungwa, ambayo hukumu yao tangu zamani haikawii, wala uvunjifu wao hausinzii.*"

Wanatembea "kwa kuufuata mwili".

2 Pet. 2:10, "*Na hasa wale waufuatao mwili katika tamaa ya mambo machafu. Na kudharau mamlaka.*"

"***Wanadharau mamlaka***"

2 Pet. 2:10 (angalia hapo juu).

"***Wakikufuru katika mambo wasiyoyajua***".

2 Pet. 2:12, "*Lakini hao kama wanyama wasio na akili, ambao walizaliwa kama wanyama tu wa kukamatwa na kupotezwa, wakikufuru katika mambo wasiyoyajua.*"

"**Wakidhania kuwa ulevi wakati wa mchana ni anasa."**

2 Pet. 2:13, "*Wakipatikana na madhara, ambo ni ujira wa udhalimu wao, wakidhania kuwa ulevi wakati wa mchana ni anasa; wamekuwa ni mawaa na aibu wakifuata anasa zisizo kiasi katika karamu zao za upendo, wafanyapo karamu pamoja nanyi.*"

"Wenye macho yajaayo uzinzi, watu wasiokoma kutenda dhambi."

2 Pet. 2:14, "*Wenye macho yajaayo uzinzi, watu wasiokoma kutenda dhambi, wenye kuhadaa roho zisizo imara, wenye mioyo iliyozoezwa kutamani, wana wa laana.*"

"Wenye mioyo iliyozoezwa kutamani".

2 Pet. 2:14 (tazama hapo juu).

Hivyo, waalimu hawa wanaoahidi uhuru wenyewe ni…

- "wameshindwa"
- "Wameletwa utumwani".

Hakika, ni wabaya zaidi sasa kuliko zamani.

2 Pet. 2:20-22, "*Kwa maana wale waliokwisha kuyakimbia machafuko ya dunia kwa kumjua Bwana na Mwokozi Yesu Kristo, kama wakinaswa tena na kushindwa, hali yao ya mwisho imekuwa mbaya kuliko ile ya mwanzo. Maana ingekuwa heri kwao kama wasingaliijua njia ya haki, kuliko kuijua kisha kuiacha ile amri takatifu waliopewa. Lakini imetukia kwao sawasawa na ile mithali ya kweli, Mbwa ameyarudia matapiko yake mwenyewe na nguruwe aliyeoshwa amerudi kugaagaa matopeni.*

Hali yao ya mwisho imekuwa mbaya kuliko ile ya kwanza.

Ingekuwa heri kwao kama wasingaliijua njia ya haki. Luka 12:47-48, "*Na mtumwa yule aliyejua mapenzi ya bwana wake, asijiweke tayari, wala kuyatenda mapenzi yake, atapigwa sana. Na yule asiyejua, naye amefanya yastahiliyo mapigo, atapigwa kidogo. Na kila aliyepewa vingi, kwake huyo vitakuwa vingi; naye waliyemwekea amana vitu vingi, kwake huyo watataka zaidi.*

Wamekuwa kama mbwa aliyerudia matapishi yake, na nguruwe aliyeoshwa kurudi kugaagaa matopeni!

Mistari hii mitatu ya mwisho inatowa swali ambalo litajibiwa hapo chini.

Waongo kwa mifumo na ahadi, tunaweza kushukuru ni kwa nini Petro angeweza kuchukuwa muda mwingi akionya kuwahusu.

Kabla ya kuhitimisha somo hili, itakuwa bora kama tukijaribu kujibu maswali mawili ambayo mara nyingi hutolewa na umakini wa Petro kuhusu waalimu wa uongo.

Maswali ya kuhitimisha

Je hawa waalimu wa uongo hapo awali walikuwa Wakristo wa kweli?

2 Pet. 2:1, "*Lakini kuliondokea manabii wa uongo katika wale watu, kama vile kwenu kutakavyokuwako waalimu wa uongo, watakaoingiza kwa werevu uzushi wa kupoteza, wakimkana hata Bwana aliyewanunua, wakijiletea uharibifu usiokawia.*"

Walikuwa "wanamkana Bwana aliyewanunua".

Hizi ni nafsi ambazo kwa wakati fulani "zilinunuliwa na Bwana".

Petro alikuwa ameandika katika waraka wake wa kwanza kwamba tunakombolewa (nunuliwa) kwa damu ya thamani ya Kristo.

1 Pet. 1:18-19, "*Nanyi fahamuni kwamba mlikombolewa si kwa vitu viharibikavyo, kwa fedha au dhahabu; mpate kutoka katika mwenendo wenu usiofaa mlioupokea kutoka kwa baba zenu; bali kwa damu ya thamani, kama ya mwana kondoo asiye na ila, asiye na waa, yaani Kristo.*"

Hivyo, hizi ni nafsi ambazo wakati fulani "walinunuliwa kwa damu".

2 Pet. 2:15, "*Wakiiacha njia iliyonyooka , wakapotea, wakiifuata njia ya Balaamu, mwana wa Beori, aliyependa ujira wa udhalimu.*"

Wameacha njia sahihi na kupotoka.

Maana hapa ni kwamba walikuwa katika njia sahihi.

Inawezekana kukiacha kitu ambacho hujawahi kuwa nacho, au kupotoka kama kila mara umekuwa ukipotea.

2 Pet. 2:20, "*Kwa maana wale waliokwisha kuyakimbia machafu ya dunia kwa kumjua Bwana na Mwokozi Yesu Kristo, kama wakinaswa tena na kushindwa, hali yao ya mwisho imekuwa mbaya kuliko ile ya kwanza.*"

Kwa muda fulani waliyakimbia machafuko ya dunia, lakini sasa walikuwa wakiitwa waalimu wa uongo.

Kumbuka kwamba “ujuzi huu” inajumuisha vitu kama ilivyoorodheshwa katika:

2 Pet. 1:5-8, “*Naam, na kwa sababu iyo hiyo mkijitahidi sana kwa upande wenu, katika imani yenu tieni na wema, na katika wema wenu maarifa, na katika maarifa yenu kiasi, na katika kiasi chenu saburi, na katika saburi yenu utauwa, na katika utauwa wenu upendano wa ndugu, na katika upendano wa ndugu, upendo. Maana mambo hayo yakiwa kwenu na kujaa tele, yawafanya ninyi kuwa si wavivu wala si watu wasio na matunda, kwa kumjua Bwana wetu Yesu Kristo.*”

Katika hivi “ujuzi iokoayo”, alafu wakakimbia, bali sasa wanatumikishwa.

2 Pet. 2:22, “*Lakini imetukia kwao sawasawa na ile mithali ya kweli, Mbwa ameyarudia matapiko yake mwenyewe, na nguruwe aliyeoshwa amerudi kugaagaa matopeni.*”

Wao, kama mbwa, wameyarudia yale ambayo walikuwa wameshayaacha kwa wakati fulani, na kuwa kama nguruwe aliyeoshwa kurudi kugaagaa matopeni.

Baadhi ya watu wanajaribu kusema kwamba hii mithali inafunua kwamba waalimu hawa wa uongo kila mara walikuwa “mbwa” na “nguruwe” hakika hawakubadilika kutoka ndani, ambayo inaelezea kurudi kwao katika matapishi na matopeni.

Lakini kwa kujuisha mazingira ya kifungu hiki, ambao wanaonekana kupoteza makusudi ya mithali.

Hakika, swali kuhusu waalimu hawa wa uongo kwamba walikuwa Wakrito wa kweli kwa wakati fulani inatuongoza sahihi katika swali lingine…

Mkristo anaweza kutenda dhambi na hivyo kupotea?

Kama “waalimu hawa wa uongo” awali walikuwa Wakristo wa kweli, jibu liko wazi “ndiyo”, kwa sababu zingatia mwisho wao:

- 2 Pet. 2:1, “*Lakini kuliondokea manabii wa uongo katika wale watu, kama vile kwenu kutakavyokuwako waalimu wa uongo, watakaoingiza kwa werevu uzushi wa kupoteza, wakimkana hata Bwana aliyewanunua, wakijiletea uharibifu usiokawia.*”
- 2 Pet. 2:3, “*Na katika kutamani watajipatia faida kwenu kwa maneno yaliyotungwa; ambao hukumu yao tangu zamani haikawii, wala uvunjifu wao hausinzii.*”

- 2 Pet. 2:17, "*Hawa ni visima visivyo na maji, na mawingu yachukuliwayo na tufani, ambao weusi wa giza ni akiba waliyowekewa.*"

Kama jibu ni "hapana", sasa kwa nini Petro anaonya katika waraka huu?

Kwa nini awaonye wale ambao "wamewakimbia wale wanaoishi katika makosa", kama hakuna hatari halisi ya kuja "kushindwa" na kuletwa "utumwani" tena? (2 Pet. 2:18-19).

Kwa nini onyo la hitimisho "jihadharini nanyi msije mkaanguka kutoka katika uimara wenu, mkiongozwa vibaya na makosa ya waovu", kama ni rahisi kwa Mkristo kuanguka? (2 Pet. 3:17).

Lakini vipi kuhusu mistari ile inayotoa ahadi ya ulinzi kwa waaminio?

Yoh. 10:28-29, "*Nami nawapa uzima wa milele; wala hawatapotea kamwe, wala hakuna mtu atakayewapokonya katika mkono wangu. Baba yangu aliyenipa hao ni mkuu kuliko wote; wala hakuna mtu awezaye kuwapokonya katika mkono wa Baba yangu.*"

Vifungu kama hivi vinatoa ahadi ya uhakika kwa "waaminio", (yule anayebaki mwaminifu; kama tukibaki kuwa waaminifu, wokovu wetu uko salama).

Ufu. 2:10, "*Usiogope mambo yatakayokupata; tazama huyo ibilisi atawatupa baadhi yenu gerezani ili wajaribiwe, nanyi mtakuwa na dhiki siku kumi. Uwe mwaminifu hata kufa, nami nitakupa taji ya uzima.*"

Lakini Biblia inaonya wazi kwamba "muumini" anaweza kujenga moyo muovu wa "kutoamini"; hiyo inaweza kutokea, ahadi ya uhakika imetumika.

Ebr. 3: 12-4:2, "*Angalieni ndugu zangu usiwe katika mmoja wenu moyo mbovu wa kutokuamini, kwa kujitenga na Mungu aliye hai. Lakini mwonyane kila siku, maadamu iitwapo leo; ili mmoja wenu asifanywe mgumu kwa udanganyifu wa dhambi. Kwa maana tumekuwa washirika wa Kristo, kama tukishikamana na mwanzo wa uthabiti wetu kwa nguvu mpaka mwisho; hapo inenwapo, leo kama mtaisikia sauti yake, msifanye migumu mioyo yenu, kama wakati wa kukasirisha. Maana ni akina nani waliokasirisha, waliposikia? Si wale wote waliotoka Misri wakiongozwa na Musa? Tena ni akina nani aliochukizwa nao miaka arobaini? Si wale waliokosa, ambao mizoga yao ilianguka katika jangwa? Tena ni akina nani aliyowaapia ya kwamba hawataingia katika raha yake, ila wale walioasi? Basi twaona ya kuwa hawakuweza kuingia kwa sababu ya kutokuamini kwao. Basi, ikiwa ikaliko ahadi ya kuingia katika raha yake, na tuogope mmoja wenu asije akaonekana ameikosa. Maana ni kweli, sisi nasi tumehubiriwa habari njema vile vile kama hao. Lakini neno lile*

lililosikiwa halikuwafaa hao, kwa sababu halikuchanganyika na imani ndani yao waliosikia."

Mwisho

Uwezekano huu alisi wa kupotoka na mtu kuukosa wokovu inatusaidia kuelewa kama jinsi ilivyoelezwa na Petro katika waraka wake.

- Anaamini kwamba Wakristo wanaweza "kuanguka kutoka katika uimara".
- Anaamini Wakristo wanaweza "kupotoswa na makosa ya waovu".

Kwa sababu hizi anachukuwa muda mwingi kuelezea "waalimu wa uongo" ambao wanapoteza wokovu wao na kujaribu kuwachukuwa wengine waungane!

Lakini kama tunaweza kukumbuka ambacho Petro anasema kuhusu…

- Maangamizi ya waalimu wa uongo.
- Machafuko ya waalimu wa uongo.
- Uharibifu wa waalimu wa uongo.
- Udanganyifu wa waalimu wa uongo.

…basi hatufanani na kuvutwa na watu kama hao.